ISSN 0856—034X

Supplement No. 34 ***4th September, 2015***

SUBSIDIARY LEGISLATION

to the Gazette of the United Republic of Tanzania No.36 Vol. 96 dated 3th September, 2015
Printed by the Government Printer Dar es Salaam by Order of Government

Tangazo la Serikali Na 359 La Tarehe 4/9/2015

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA 290)

_____

SHERIA NDOGO

_____

(Zimetungwa Chini ya Kifungu cha 6 (1) NA 16(1)

_____

SHERIA NDOGO ZA MAREKEBISHO (ADA NA USHURU)(MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA TABORA, 2014

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru)(Marekebisho) za Halmashauri ya Manispaa ya Tabora za mwaka, 2014 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika maeneo yote yaliyo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

3. Katika Sheria Ndogo hizi:-

"Ada ya Ushuru" Maana yake ni Malipo yanayotozwa na Halmashauri kwa ajili ya shughuli mbalimbali

zinazoendeshwa ndani ya Halmashauri;

"Halmashauri" Maana yake Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

"Manispaa" Maana yake ni sehemu yoyote ya ardhi iliyo ndani ya mipaka ya Manispaa Tabora

"Maegesho" Maana yake eneo lolote lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya maegesho ya magari makubwa na madogo.

"Mkurugenzi" Ina maana ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora.

"Wakala" Maana yake ni mtu, Kampuni binafsi au asasi ya Umma au binafsi iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya ada na ushuru kwa niaba yake.

4.-(1) (i) Kutakuwa na ada ya ushuru utakaotozwa kutoka katika vyanzo vya mapato vilivyoainishwa katika Sheria ndogo hizi.

(ii) Ada na ushuru utakaokusanywa chini ya sheria ndogo hizi zitatumika kwa ajili ya shughuli za maendeleo ambazo zitainufaisha jamii ya Halmashauri ya Manispaa Tabora.

(iii) Ada na ushuru utakaokusanywa chini ya sheria ndogo hizi utakusanywa na Halmashauri au Wakala aliyeteuliwa na Halmashauri.

5. Ada na ushuru utatozwa chini ya Sheria ndogo hizi unaweza kulipwa kwa:

(a) Kila siku ya wiki husika kwa pande wa ushuru wa maegesho ya magari na ukusanyaji ushuru wa maliasili.

(b) Kila mwezi katika siku ya kwanza ya mwezi husika kwa tozo la ada ya vibali mbalimbali isipokuwa kama siku iliyotajwa itakuwa ni siku ya Sikukuu.

(2) Itakuwa ni wajibu wa Wakala:-

(a) Kumpatia risiti mtu yeyote aliyelipa ada na ushuru;

(b) Kuandaa taarifa ya mapato ya kila mwezi na kuziwasilisha Halmashauri akionyesha kiasi cha mapato yaliyokusanywa;

(3) Wakala yeyote ambaye:-

a) Atashindwa kukabidhi kiasi chochote cha fedha alizokusanya kama ushuru wa Halmashauri, atakuwa ametenda kosa na atatozwa adhabu ya asilimia ishirini na tano (25%) ya pesa alizotakiwa kukabidhi/kuwasilisha;

b) Hataruhusiwa kumdai mtu yeyote kiasi kinachozidi kiwango cha ushuru kilichowekwa na sheria ndogo hizi;

c) Kwa uzembe au makusudi akitoa taarifa za mapato zenye makosa, iwe kwa mdomo au kwa maandishi, kuhusu idadi ya waliolipa kodi au jumla ya malipo aliyokusanya au kupokea atakuwa ametenda kosa na atafikishwa kwenye Mahakama yenye Mamlaka ya kuendesha mashauri ya madai;

d) Sheria ndogo hizi hazizuii au hazimwondolei mtu yeyote kosa la jinai chini ya Sheria za nchi kwa mtu yeyote atayepatikana na hatia ya uzembe wa kutolipa au kutowasilisha mapato ya Halmashauri.

6. Endapo Halmashauri ya Manispaa Tabora itaongeza viwango vya Ada na Ushuru katika kitu chochote

kilichoorodheshwa kwenye kiambatanisho, Halmashauri itarekebisha viwango hivyo kwa kuzingatia marekebisho yaliyofanyika.

KIAMBATISHO – ADA NA USHURU
I: VIBALI

Kibali cha kukusanya Maliasili	Tshs.30,000/= kwa mwezi
Kibali cha kuuuza mazao ya chakula	Tshs.20,000/= kwa mwezi
Kibali cha kuuza samaki	Tshs. 20,000/= kwa mwezi

II: MALIASILI

Mchanga kwa kila mita ya ujazo (M^3)	Tshs.1000/= kwa kila mita ya ujazo
Moramu kwa kila mita ya ujazo (M^3)	Tshs.1,800/= kwa kila mita ya ujazo
Kokoto kwa kila mita ya ujazo (M^3)	Tshs. 1,800/= kwa kila mita ya ujazo
Mawe kwa kila mita ya ujazo (M^3)	Tshs. 1,800/= kwa kila mita ya ujazo

III: MAEGESHO – IPULI

Magari madogo (tani 3 – tani 6)	Tshs.2,000/= kwa siku
Malori (tani 7 tani 15)	Tshs.5,000/= kwa kila siku
Malori makubwa (tani 15 – tani 30)	Tshs. 8,000/= kwa kila siku
Malori (zaidi ya tani 30)	Tshs. 10,000/= kwa kila siku

IV: ENEO LA MNADA – IPULI

Nyama ya Mbuzi (Wachinjaji)	Tshs.500/= kwa kila siku ya Mnada
Nyama choma kwa jiko	Tshs.1,000/= kwa kila siku ya Mnada
Vinywaji (Bia, Soda na maji)	Tshs. 1,000/= kwa kila siku ya Mnada
Mama Lishe	Tshs. 500/= kwa kila siku ya Mnada
Pombe za kienyeji	Tshs. 500/= kwa kila siku ya Mnada
Bidhaa za Nguo na Vyombo	Tshs. 1,000/= kwa kila siku ya Mnada
Bidhaa ndogondogo za kuweka chini	Tshs. 500/= kwa kila siku ya Mnada

V: NGOZI ZA WANYAMA:

Ngozi ya N'gombe	Tshs.500/= kwa ng'ombe mmoja
Ngozi ya mbuzi	Tshs.300/= kwa mbuzi mmoja
Ngozi ya kondoo	Tshs. 300/= kwa kondoo mmoja

VI: ADA YA KUTUMIA VIFAA VYA HALMASHAURI:

Na.	**Aina**	**Kiwango cha Ada**
1)	Kutumia Lori la Halmashauri	Tshs. 120,000/= kwa siku
2)	Kutumia ukumbi wa Halmashauri	Tshs. 200,000/= kwa siku
3)	Kutumia Grader la Halmashauri	Tshs. 125,000/= kwa saa
4)	Kutumia Roller la Halmashauri	Tshs. 75,000/= kwa saa

VII: ADA YA MABANGO STANDI MPYA

Kutangaza kwa kutumia spika	Tshs.2,000/= kwa siku

Kufutwa

7. Sehemu 'S' (vii) na 'U' ya Sheria Ndogo za Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa Tabora za mwaka 1998 zimefutwa.

8. Sehemu ya 3 ya sheria ndogo za (uchimbaji na ushuru wa ngozi) ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora mwaka 1998 imefutwa.